CELEBRATION DE MARIAGE

# PREPARONS LE DIMANCHE

LIVRET HEBDOMADAIRE DES PARTITIONS

IBADA YA NDOA

†

©Partitions ++, Février 2026

# NENO LA MUNGU

## KATIKA IBADA YA

# NDOA
# TAKATIFU

Commission de Liturgie pour le Swahili, Zaïre
1972

# IV. ZABURI

**Zaburi 32 : Maongozi ya Mungu** 32, 12 na 18, 20-21, 22.

K/ **Dunia imejaa wema wake Bwana (5 b).**

12 Heri taifa lenye Bwana ni Mungu wake,
kabila alilochagua kuwa urisi wake.

18 Macho ya Bwana yameelekea wenye kumcha,
wale wenye kutumainia wema wake.

20 Roho yetu inamngojea Bwana,
Yeye ndiye msaada wetu na ngao yetu.

21 Kweli moyo wetu unafurahiwa kwake,
twategemea jina lake takatifu.

22 Huruma yako, ee Bwana, itushukie,
kama vile tunavyokutumainia !

2. **Zaburi 33 : Bwana ni mwema kwa sisi wote**
33, 2-3, 4-5, 6-7, 8-9.

K/ **Nitamtukuza Bwana kila wakati (2a).**

ao K/ **Onjeni, mwone jinsi Bwana alivyo mwema (9a).**

2 Nitamtukuza Bwana kila wakati;
sifa yake kinywani mwangu sikuzote.

3 Roho yangu ijisifu katika Bwana:
wanyonge wasikie na kufurahi.

4 Mtukuzeni Bwana pamoja nami;
tulikuze jina lake wote pamoja.

5 Nalimkimbilia Bwana, akanisikiliza,
akaniopoa katika hofu zangu zote.

6 Mtazameni Yeye na mfurahiwe,
wala nyuso zenu zisihuzunike.

7 Mnyonge huyu alilia, naye Bwana akasikia,
akamwokoa katika shida zake zote.

8 Malaika wa Bwana amepanga jeshi
kando zote za wenye kumcha, akawaopoa.

9 Onjeni, mwone jinsi Bwana alivyo mwema;
heri mtu yule anayemkimbilia.

3. **Zaburi 102 : Mungu ni mwema 102, 1-2, 8 na 13, 17-18a.**

K/ **Bwana ni mwenye huruma na upole (8a).**

ao K/ **Wema wa Bwana kwa wenye kumcha,**
**wadumu tangu milele hata milele (17).**

Umsifu Bwana, ee roho yangu,
na yote yaliyo ndani mwangu, jina lake takatifu !

2 Umsifu Bwana, ee roho yangu,
wala usisahau mema yake yote !

8 Bwana ni mwenye huruma na upole,
mvumilivu na mwingi wa wema.

13 Kama vile baba anavyowahurumia watoto wake,
ndivyo Bwana anavyowahurumia wenye kumcha.

17 Wema wa Bwana kwa wenye kumcha,
wadumu tangu milele hata milele,
na haki yake kwa waana wa waana wao,
18 kwa wale wanaoshika agano lake.

**4. Zaburi 111 : Heri ya mtu mwema. 11, 1-2, 3-4, 5-7a, 7bc-8, ⁽**

**K/ Heri mtu anayependezwa sana na amri za Bwana (1b)**
ao **K/ Aleluya.**

1 Heri mtu mwenye kumheshimu Bwana,
anayependezwa sana na amri zake !
2 Katika nchi wazao wake watakuwa wenye nguvu,
kizazi cha waamini kinabarikiwa.

3 Mali na utajiri nyumbani mwake,
na haki yake yakaa milele.
4 Gizani Mwanga unawatokea waamini:
Mpole, Wenye huruma na haki.

5 Ni mwema mtu anayehurumia na kukopesha,
anayetengeneza mambo yake kwa haki.
6 Kwani hatatikisika milele,
mtu mwema atakumbukwa milele.

7 Hataogopa habari mbaya;
moyo wake wamtumaini Bwana kwa imara.
8 Moyo wake ni sabiti, hauogopi kitu,
mpaka awaone adui zake wamepata haya.

9 Anagawa, anawagawia maskini,
haki yake yakaa milele;
pembe yake itainuka kwa sifa.

5. **Zaburi 127 : Heri ya jamaa njema.** 127, 1-2, 3, 4-5

K/ **Heri mtu anayemheshimu Bwana (1).**

ao K/ **Ndivyo anavyobarikiwa mtu**
**mwenye kumheshimu Bwana (4)**

1 Heri mtu anayemheshimu Bwana,
anayeenda katika njia zake !

2 Kwa taabu ya mikono yako utashiba,
utaona heri na raha.

3 Mke wako kama mzabibu mzazi
ndani ya nyumba yako;

waana wako kama miche ya mizeituni,
wakizunguka meza yako.

4 Ndivyo anavyobarikiwa mtu
mwenye kumheshimu Bwana !

5 Bwana akubariki toka Sioni:
uone usitawi wa Yerusalemu
siku zote za maisha yako !

6. Zaburi 144 : Ukubwa na wema wa Mungu;
144, 8-9, 10 + 15, 17-18

K/ **Bwana ni mwema kwa wote (9a)**

8 Bwana ni mwenye huruma na mpole,
mvumilivu na mwingi wa wema.

9 Bwana ni mwema kwa wote,
huruma yake juu ya kazi zake zote.

10 Matendo yako yote yanakutukuza, ee Bwana,
na waamini wako wanakusifu.

15 Macho ya wote yanakutumainia,
nawe unawapa chakula wakati wake.

17 Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote,
na mwema katika matendo yake yote.

18 Bwana ni karibu na wote wanaomwita,
wote wanaomwita kwa uaminifu.

7. **Zaburi 148: Mbingu na dunia zimsifu Bwana**
**148, 1-2, 3-4, 9-10, 11-12ab,12c - 14a.**

**K/ Wote wasifu jina la Bwana (12c)**
ao **K/ Aleluya.**

1 Msifuni Bwana toka mbinguni,
msifuni mahali pa juu;
2 msifuni, enyi malaika wake wote,
msifuni, enyi majeshi yake yote !

3 Msifuni, jua na mwezi,
msifuni, nyota zote zenye kungara;
4 msifuni, mbingu za mbingu,
na maji yaliyo juu ya uwingu.

9 Enyi milima na vilima vyote,
miti na matunda na mierezi yote;
10 wanyama wa mwitu na wanyama wa kufugwa,
nao wanaotambaa chini, na ndege wenye mabawa.

11 Enyi wafalme wa dunia na makabila yote,
wakuu na waamuzi wote wa dunia;
12 vijana waume na mabinti,
wazee pamoja na watoto.

Wasifu jina la Bwana,
13 maana jina lake ni kubwa peke yake;
utukufu wake wapita dunia na mbingu,
14 amekuza pembe ya kabila lake.

## V. ALELUYA NA WIMBO MBELE YA ENJILI

1. Kila mmoja anayependa
amezaliwa na Mungu,
naye anamjua Mungu (1 Yoa. 4, 7b).

2. Mungu ni mapendo:
tupendane, kama Mungu alivyotupenda
(1 Yoa. 4, 8 na 11).

3. Tukipendana, Mungu akaa ndani yetu,
na mapendo yake yametimilika ndani yetu.
(1 Yoa. 4, 12).

4. Anayekaa katika mapendo,
akaa ndani ya Mungu,
naye Mungu akaa ndani yake. (1 Yoa. 4, 16).

# PSAUMES

## Zaburi

# DUNIA IMEJAA



Mtunzi : Charles NYENZE
Maneno : Zaburi 32




# BWANA NI MWENYE HURUMA

*Misa ya ndoa*

**Mus: Parfait KAKULE KA.**
**Chorale Saint Benoît de Goma**

***Zab 102,1-2,3-4,8 na 10,12-13***






*Parfait KAKULE KA. Goma, 23/01/2025*

# NITAMTUKUZA BWANA

***Mus: Parfait KAKULE KA.***
***Chorale diocésaine de Goma***

***Zab 33, Misa ya ndoa***
***Itaimbwa ingawa walisoma katika kitabu cha   Tobiti 8:5-10***




1. Nitamtukuza Bwana kila wakati ;
sifa yake kinywani mwangu siku zote.
Roho yangu ijisifu katika Bwana :
wanyonge wasikie na kufurahi.

2. Mtukuzeni Bwana pamoja nami ;
Tulikuze jina lake wote pamoja.
Nalimkimbilia Bwana, akanisikiliza,
Akaniopoa katika hofu zangu zote.

3. Mtazameni Yeye mkafurahiwe,
Wala nyuso zenu zisihuzunike.
Mnyonge huyu alilia, naye Bwana akasikia,
Akamwokoa katika shida zake zote.

# Heri mtu anayemheshimu Bwana

***Misa ya ndoa***

***Zab 127***

***Mus: Parfait KAKULE KA.***
***Chorale Saint Benoît de Goma***




***Parfait KAKULE KA. Goma, décembre 2019***

# WATU WAKO WATAKUWA WATU WANGU

*A l'occasion du Mariage de Parfait KAKULE et EMILIENNE NZIGIRE du 26/12/2018*

***Musique: Parfait KAKULE KA.***

***Texte refrain: Ruth 1.16-17; Couples: Psaume 127***




*Copyright by Ngashani Dieu-merci NGADI*

# Wote wasifu jina ya Bwana

Ibada ya Ndoa Takatifu

Texte: Zaburi 148,1-2,3-4,9-10,11-12ab,12c-14a

Musique: Rodriguez NTUGULO




1. (a) Msifuni Bwana toka mbinguni.
Msifuni mahali pa juu.
(b) Msifuni, enyi malaika wake wote.
Msifuni, enyi majeshi yake yote.
2. (a) Msifuni, jua na mwezi,
Msifuni, nyota zote zenye kungara.
(b) Msifuni, mbingu na dunia,
Na maji yaliyo juu ya uwingu.
3. (a) Enyi milima na vilima vyote,
miti yaliyo juu ya uwingu.
(b) Wanyama wa mwitu na wanyama wa kufugwa,
nao wanaotambaa chini, na ndege wenye mabawa.
4. (a) Enyi wafalme wa dunia na makabila yote,
wakuu na waamuzi wote wa dunia.
(b) Vijana wauma na mabinti,
wazee pamoja na watoto.
5. (a) Wasifu jina la Bwana,
maana jina lake ni kubwa peke yake.
(b) Utukufu wake wapita dunia na mbingu,
amekuza pembe ya kabila lake.

# WOTE WASIFU JINA LA BWANA


## Zaburi katika Misa ya Ndoa Takatifu


Neno: Zab. 148, 1-4. 9-10
Mtungaji: Olivier BAHATI



# *Zaburi 127*
# *Heri ya jamaa njema*

**Musique: Stéphane DHEDJO**







1. Heri mtu anavyomheshi***mu*** ***Bwana***,
   anayeenda katika njia ***zake***!
   Kwataabu na mikono yako u***tashiba***,
   utaona heri ***na*** ***raha***.


2. Mke wako kwama mzabi***bu*** ***mzazi***
   ndani ya nyumba ***yako***;
   waana wako kama miche ya mize***ituni***,
   wakizunguka ***me***za ***yako***.

3. Ndivyo anavyobarikiwa mtumwenye kumheshi***mu*** ***Bwana***!
   Bwana akubariki toka Si***on***i:
   uone usitawi wa Yeru***salemu***
   siku zote za ma***i***sha ***yako***

# Zaburi 148

### *Mbingu na dunia zimsifu Bwana*

Musique: Stéphane DHEDJO




**1. Msifuni Bwana toka mbinguni,**
**msifuni mahali pa juu;**
**msifuni, enyi malaika wake wote,**
**msifuni, enyi majeshi yake yote!**

**2. Msifuni, jua na mwezi,**
**msifuni, nyota zote zenye kungara;**
**msifuni, mbingu za mbingu,**
**na maji yaliyo juu ya uwingu.**

**3. Enyi milima na vilima vyote,**
**miti na matunda na mierezi yote;**
**wanyama wa mwitu na wanyama wa kufungwa,**
**nao wanaotambaa chini na ndege wenye mabawa.**


**4. Enyi wafalme wa dunia na wakabila yote,**
**Wakuu na waamuzi wote wa dunia;**
**vijana waume na mabinti,**
**wazee pamoja na watoto.**

**5. Wasifu jina la Bwana,**
**maana jina lake ni kubwa peke yake;**
**utukufu wake wapita dunia na mbinguni,**
**amekuza pembe ya kabila lake.**

# Zaburi 144

## *Ukubwa na wema wa Mungu*

**Musique : Stéphane DHEDJO**







1. Bwana ni mwenye huruma na ***mpole,***
   mvumulivu na mwingi wa ***wema***.
   Bwana ni mwema kwa ***wote***,
   huruma yake juu ya kazi zake ***zote***.

2. Matendo yako yote yanakutukuza, ee ***Bwana***,
   na waamini wako wanaku***sifu***.
   Macho ya wote yanakutumai***nia***,
   nawe unawapa chakula wakati ***wake***.

3. Bwana ni mwenye haki katika njia zake ***zote***,
   na mwema katika matendo yake ***yote***.
   Bwana ni karibu na wote wanaom***wita***,
   wote wanaomwita kwa uamini***fu***.


# *Zaburi 32*
## *Maongozi ya Mungu*

Musique: Stéphane DHEDJO



# ONJENI MUONE

Musique: Innocent BISHIKWABO
Texte: Psaume 33




# BWANA NI MWENYE HURUMA

**Zaburi 102 / Katika Misa ya Ndoa**

**Musique: Innocent BISHIKWABO**







1. U - msi - fu Bwa - na ee Ro - ho ya - ngu,
U - msi - fu Bwa - na ee Ro - ho ya - ngu,

2. Ye - ye a - sa - me - he za - mbi za - ko,
Ye - ye a - ko - mbo - a u - zi - ma,

3. Bwa - na ni mwe - nye hu - ru - ma,
Hu - te - ndi kwa ka - di - ri ya za - mbi,

4. Kama ma - sha - ri - ki i - li - vyo mwa - li,
Kama vi - le Ba - ba a - na - hu - rumi - ya,



1. na yo - te ya - li - yo nda - ni ya-ngu, ji - na la - ke ta - ka - ti - fu.
Wa - la u - si - sa - ha - u me-ma, me-ma ya - ke yo - te.

2. a - po-nya ma-go-njwa ya - ko yo - te, ma-go-njwa ya-ko yo - te.
a - na-ku-zu-ngu-sha kwa we-ma, kwa we-ma na re-he - ma.

3. mvu-mi-li-vu na mwi-ngi wa we-ma, na - mwi-ngi wa we - ma.
wa - la hu-ta pa-ti - li - zi, kwa ma-ko-sa ye - tu.

4. vi - vyo na za-mbi ze-tu zo - te, a-me zi-we-ka mba - li.
Hi - vyo Bwa-na a-wa-hu - ru-mi-a, wa-tu we-ma wo - te.

# HERI MTU ANAYEPENDEZWA

*(Mariage)*

Texte tiré de *Neno la Mungu katika Ibada ya ndoa takatifu*

**Musique : Charles NYENZE**
**Texte : Zaburi 111**




19
na, a - na - ye - pe - nde - zwa sa - na - na - am - ri za -
ke, na - ha - ki - ya - ke - ya - ka - a mi - le -
sha, a - na - ye - te - nge - ne - za ma - mbo ya - ke kwa ha -
ya; mo - yo wa - ke u - nam - tu - ma - i - ni - a Bwa - na kwa i - ma -
wa, a - na - wa - ga - wi - a - mas - ki -
23
ke! Ka - ti - ka nchi wa - za - o wa - ke wa - ta - ku - wa we - nye ngu -
le. Gi - za - ni mwa - nga u - na - wa - to - ke - a wa - a - mi -
ki. Kwa - ni - ha - ta - ti - ki - si - ka - mi - le -
ra. Mo - yo wa - ke ni sa - bi - ti ha - u - o - go - pe - ki -
ni, ha - ki - ya - ke - ya - ka - mi - le -
27
vu, ki - za - zi cha wa - a - mi - ni ki - ta - ba - ri - ki - wa.
ni: m - po - le, we - nye hu - ru - ma na - ha - ki.
le, mtu mwe - ma a - ta - ku - mbu - ka mi - le - le.
tu, mpa - ka a - o - ne a - du - i za - ke wa - me - pa - ta ha - ya.
le; pe - mbe - ya - ke i - ta - i - nu - ka kwa - si - fa.

# BWANA NI MWEMA

**Musique : Charles NYENZE**
**Texte : Zaburi 144**




*1.Bwana ni mwenye huruma na mpole*
*mvumilivu na mwingi wa wema.*
*Bwana ni mwema kwa wote,*
*huruma yake juu ya kazi zake zote.*

*2.Matendo yako yote yanakutukuza, ee Bwana,*
*na waamini wako wanakusifu.*
*Macho ya wote yanakutumainia,*
*nawe unawapa chakula wakati yake.*


*3.Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote,*
*na mwema katika matendo yake yote.*
*Bwana ni karibu na wote wanaomwita,*
*wote wanaomwita kwa uaminifu.*

# ONJENI MWONE

***(Mariage)***

**Musique : Charles NYENZE**

**Texte : Zab 33**




1. Nitamtukuza Bwana kila wakati;
sifa yake kinywani mwangu siku zote
Roho yangu ijisifu katika Bwana:
wanyonge wasikie na kufurahi.

2.Macho ya Bwana yawaangalia watenda mema,
na masikio yake yaelekea milio yao.
Uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya,
ili angoe ukumbusho wa duniani.

3.Watu xema wameita , naye Bwana awasikiliza,
awaopoa katika shida zao zote.
Bwana yupo karibu nao waliopondeka moyo,
awaokoa wenye kuvunjika roho.
4.Mateso ya mtu mwema ni mengi,
lakini Bwana amwopoa katika yote
Ailinda mifupa yake yote:
hata mmoja wake hautavunjika.
5.Ubaya unamwua mtu muovu,
nao wenye kumchukia mtu mwema watapatilizwa.
Bwana anakomboa roho za watumishi wake,
wote waliomkimbilia hawatapatilizwa kamwe.

BWANA NI MWENYI HURUMA NA MPOLE
ZABURI 102

M: Achille WAKILONGO K.






AFLOW

# Dunia imejaa wema


Zaburi 32

Mus. Innocent BISHIKWABO
Katika Misa ya Ndoa



1. Heri taifa lenye Bwana ni Mu - ngu wa - ke,
2. Macho ya Bwana yanaelekea we - nye kum - cha,
3. Roho yetu inamgonje - a Bwa - na,
4. Kweli moyo wetu unafurahi - wa kwa - ke,
5. Huruma yako ee Bwana itu - shu - ki - e,




1. Kabila alilochagua kuwa u - ri - si wa - ke.
2. Wale wenye kutumainiya we - ma wa - ke.
3. Yeye aliye msaada wetu na nga - o ye - tu.
4. Twategemea jina lake ta - ka - ti - fu.
5. Kama vile tunavyo kutu - ma - i - ni - a.

# ACCLAMATION

## Shangilio ya Enjili

# ALELUYA IBADA YA NDOA

*(1Yoa. 4, 12)*

**Musique : Charles NYENZE**



# ALELUYA IBADA YA NDOA

*(1Yoa.4, 7b)*

**Musique : Charles NYENZE**



# ALLELUYA, MUNGU NI MAPENDO

Shangilio la Enjili katika Misa ya Ndoa Takatifu

Neno: 1Yn 4, 8. 11-12
Mtungaji: Olivier BAHATI




Fait au Théologat Saint Octave de Vulindi/Butembo, le 21 janvier2026.


# Aleluya tukipendana

1 Yoa. 4,12

Ibada ya Ndoa Takatifu.

Musique: Rodriguez NTUGULO




22
na ma-pe-ndo ya-ke ya-me-
4.Tu-ki-pe-nda-na, Mu-ngu a-ka-a nda-ni ye-tu,
25
ti - mi - li - ka nda - ni ye - tu.(1Yoa.4,12).